**MUHTASARI WA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI WA KUJADILI TAARIFA ZA ROBO YA I YA MWAKA 2023/2024 ULIOFANYIKA TAREHE 08/12/2023 KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI YA WILAYA YA BUNDA.**

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA**

| NA. | JINA | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Charles M. Manumbu | Diwani Kata ya Iramba - Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Keremba I. Keremba | Diwani Kata ya Nyamang'uta - Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Sumera K. Mzumari | Diwani Kata ya Hunyari - Mjumbe |
| 4. | Mhe. Fedson Rwesunga | Diwani Kata ya Nampindi - Mjumbe |
| 5. | Mhe. Nyambura Nyasonge | Diwani Kata ya Mihingo - Mjumbe |
| 6. | Mhe. Mariam W. Wambura | Diwani Viti Maalum - Mjumbe |
| 7. | Mhe. Mtamwega T. Mgaywa | Diwani Kata ya Kibara - Mjumbe |
| 8. | Mhe. Sophia B. Makamulo | Diwani Viti Maalum - Mjumbe |
| 9. | Mhe. Samwel M. Hewa | Diwani Kata ya Butimba - Mjumbe |
| 10 | Mhe. Berrynice J. Bitta | Diwani Viti Maalum - Mjumbe |
| 11 | Mhe. Mramba S. Nyamkinda | Diwani Kata ya Ketare - Mjumbe |
| 12 | Mhe. Emmanuel M. Makoba | Diwani Kata ya Salama - Mjumbe |
| 13 | Mhe. Mganga G. Jongora | Diwani Kata ya Mugeta - Mjumbe |
| 14. | Mhe. Lufunjo E. Ndaro | Diwani Kata ya Kisorya - Mjumbe |
| 15 | Mhe. Mgendi P. Kwaye | Diwani Kata ya Nyamihyolo - Mjumbe |
| 16 | Mhe. Mkama B. Mborwe | Diwani Kata ya Chitengule - Mjumbe |
| 17 | Mhe. Tatu K. Madaha | Diwani Viti Maalum - Mjumbe |
| 18 | Mhe. Edward J. Namwatta | Diwani Kata ya Nansimo - Mjumbe |
| 19 | Mhe. Ruth W. Mtani | Diwani Viti Maalum - Mjumbe |
| 20 | Mhe. Kaballa R. Maganja | Diwani Kata ya Namhula - Mjumbe |
| 21 | Mhe. Nyachiro C. Chitema | Diwani Viti Maalum - Mjumbe |
| 22 | Mhe. Kanazi Fulgence | Diwani Kata ya Kasuguti - Mjumbe |
| 23 | Mhe. Nyamkinda B. Mkama | Diwani Kata ya Igundu - Mjumbe |
| 24 | Mhe. Fortunatus Maiga | Diwani Kata ya Neruma - Mjumbe |
| 25 | Mhe. Ibrahim M. Igayi | Diwani Kata ya Nyamuswa - Mjumbe |
| 26 | Mhe. Boniphace Getere | Mbunge Jimbo la Bunda - Mjumbe |

**WAJUMBE WASIOHUDHURIA**

| NA. | JINA | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Charles M. Kajege | Mbunge Jimbo la Mwibara - Kwa taarifa |

**WATENDAJI WALIOHUDHURIA.**

| NA. | JINA KAMILI | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1 | Ndg. Changwa M. Mkwazu | Mkurugenzi Mtendaji (W) - Katibu |
| 2 | Ndg. Salum Mtelela | Katibu Tawala (W) |



CamScanner

| | | |
|---|---|---|
| 3 | Ndg. Optatus J. Lusolela | Mkuu wa Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu (W) |
| 4 | C.P.A (T) Mlowe Victory | Mkuu wa Kitengo cha Fedha na Uhasibu (W) |
| 5 | Ndg. Dickson Balige | Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango na Uratibu (W) |
| 6 | Ndg. Noel M. Shamazugu | Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii (W) |
| 7 | Ndg. Prisca M. Blase | Afisa Tarafa Chamriho |
| 8 | Ndg. Rahel P. Mdachi | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi na Ugavi (W) |
| 9 | Ndg. Nambua Semlugu | Kaimu Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari (W) |
| 10 | Ndg. Restuta P. Bakebula | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani (W) |
| 11 | Ndg. Scola Kisibo | Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Sheria (W) |
| 12 | Ndg. Samwel M. Werema | Mkuu wa Idara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji (W) |
| 13 | Ndg. Thomas Novatus Festus | Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA(W) |
| 14 | Ndg. Eustace C. Kabwogi | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Sanaa, Utamaduni na Michezo (W) |
| 15 | Ndg. Oscar Kapinga | Mkuu wa Idara ya Elimu ya Awali na Msingi (W) |
| 16 | Ndg. Colman Moshy | Mratibu TASAF (W) |
| 17 | Ndg. Marwa P. Kitende | Mkuu wa Kitengo cha Maliasili na Uhifadhi wa Mazingira (W) |
| 18 | Ndg. Maria C. Kimaro | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini (W) |
| 19 | Ndg. Johanes Bucha | Mratibu Mradi wa Mazingira (W) |
| 20 | Ndg. Oscar Nchemwa | Mkuu wa Idara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi (W) |
| 21 | Ndg. Boniphace Maiga | Kaimu Afisa Tarafa Kenkombyo na Nansimo |
| 22 | Eng. Francis Mwikeve | Kaimu Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Miundombinu Mijini na Vijijini (W) |
| 23 | Dr. Hamidu Adinani | Kaimu Mkuu wa Idara ya Afya, Ustawi wa Jamii na Huduma za Lishe (W) |
| 24 | Ndg. Mariastella Balithazar | Afisa Uchaguzi (W) |

**WAGENI WAALIKWA**

| NA. | JINA KAMILI | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1. | Dr. Vicent Anney | Mkuu wa Wilaya |
| 2. | Mhe. Mayaya A. Magese | Mwenyekiti Chama Cha Mapinduzi (W) |
| 3. | Ndg. Songoma S. Pius | RS - Mara |
| 4. | Ndg. Frank D. Marwa | JKT - Bulamba |
| 5. | Ndg. Hagai Mwakasege | Kny; OCD |
| 6. | Ndg. Hoja L. Waheke | Mshauri JA |
| 7. | Ndg. Sadikiel J. Mhomboje | DIO |
| 8. | Ndg. Yusuph R. Mkumbila SP | AG - DPO |



CamScanner

| | | |
|---|---|---|
| 9. | Eng. William Boniphace | Meneja RUWASA (W) |
| 10. | Eng. Baraka H. Mkuya | Meneja TARURA (W) |
| 11. | Ndg. Peter Selestine | Meneja TANESCO (W) |

**WAANDISHI WA HABARI**

| NA. | JINA KAMILI | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1. | Ndg. Asha Shaaban | EATV/ZBC |
| 2. | Ndg. Ghati Msamba | UHURU/MUSOMA TV |
| 3. | Ndg. Adelinus Banenwa | Mazingira FM |

**SEKRETARIETI**

| NA. | JINA KAMILI | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1. | Ndg. Pili A. Masaza | Mwandishi wa Vikao |
| 2. | Ndg. Amos J. Kaunya | Mwandishi wa Vikao |
| 3. | Ndg. Hana Mwidibo | Mwandishi wa Vikao |

**Ajenda za mkutano wa Baraza la Madiwani wa tarehe 09/03/2023**

1. Kufungua mkutano.
2. Kuridhia agenda.
3. Maswali ya papo kwa papo.
4. Hoja binafsi kufuatana na jinsi zilivyopokelewa.
5. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa mkutano wa tarehe 30/08/2023, 31/08/2023 na 05/09/2023.
6. Kupokea taarifa kutoka TARURA, mpango wa TANESCO na RUWASA.
7. Kupokea taarifa yoyote ambayo Mwenyekiti anapenda itolewe kwa Halmashauri.
8. Kupokea taarifa za Kamati za Kudumu za Halmashauri kutoka kwa Wenyeviti wa Kamati ambao watahusika kujibu maswali ya wajumbe kuhusiana na kazi za Kamati husika.
   - Taarifa ya Kamati ya Kudhibiti UKIMWI (W).
   - Taarifa ya Kamati ya Maadili ya Madiwani.
   - Taarifa ya Kamati ya Huduma za Jamii.
   - Taarifa ya Kamati ya Huduma za Uchumi.
   - Taarifa ya Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango.
9. Kupokea taarifa kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri.
10. Kufunga mkutano.

**MUHTASARI NA. HWB/2022 2023/01/01 KUFUNGUA MKUTANO**

1.1 Katibu alimkaribisha Mwenyekiti afungue mkutano.

1.2 Mwenyekiti kabla hajafungua mkutano, alitambua uwepo wa wajumbe wa mkutano, wataalam pamoja na wageni waalikwa wakiwemo Waandishi wa Habari pamoja na Kamati ya Ulinzi na Usalama na wengineo.

1.2.1 Alisema kuwa, mkutano huo ulikuwa ufanyike tarehe 16/11/2023 na kuahirishwa baada ya wajumbe kumuagiza Mkurugenzi Mtendaji (W) afanye

ukaguzi wa fedha zilizotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi (BCRAP) na katika mkutano huo alikuwa ametekeleza agizo hilo.

1.2.2 Alisema kuwa kwa kuwa wajumbe walikaa na makabrasha ya mkutano kwa muda mrefu, hivyo kila mjumbe atatumia dakika mbili (02) kutoa hoja yake.

1.2.3 Alikemea lugha za kejeli na vijembe wakati wa majadiliano, alisema kuwa hazitakuwa na nafasi kwenye mkutano huo na hata mikutano na vikao vinavyofuata.

1.2.4 Alifungua mkutano saa 06:08 mchana.

**MUHTASARI NA. HWB/2022 2023/01/02 KURIDHIA AJENDA**

2.1 Ajenda kumi (10) ziliwasilishwa kwenye mkutano.

2.2 Wajumbe walizipokea ajenda zote kumi (10) kuwa zijadiliwe kwenye mkutano huo.

**MUHTASARI NA. HWB/2022 2023/01/03 MASWALI YA PAPO KWA PAPO.**

3.1 Mwenyekiti alisema kuwa utaratibu wa kuuliza maswali ya papo kwa papo utaendelea katika mabaraza yanayofuata.

**MUHTASARI NA. HWB/2022 2023/01/04 HOJA BINAFSI KUFUATANA NA JINSI ZILIVYOPOKELEWA.**

4.1 Mhe. Mtamwega T. Mgaywa – Diwani wa Kata ya Kibara alihoji kukosekana kwa hoja yake binafasi aliyoiwasilisha katika ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) ndani ya muda wa kikanuni.

4.1.1 Wajumbe waliagiza hoja hiyo binafsi pamoja na majibu ya hoja hiyo viwasilishwe kwenye mkutano ujao wa robo ya II ya mwaka wa fedha 2023/2024 kwa maandishi kwa ajili ya kujadiliwa.

4,2 Mhe. Sumera Kiharata Diwani wa Kata ya Hunyari alihoji pia kukosekana kwa hoja yake binafasi aliyoiwasilisha katika ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) ndani ya muda wa kikanuni.

4.2.1 Wajumbe waliagiza hoja hiyo binafsi pamoja na majibu ya hoja viwasilishwe kwenye mkutano ujao wa robo ya II ya mwaka wa fedha 2023/2024 kwa maandishi kwa ajili ya kujadiliwa.

**MUHTASARI NA. HWB/2022 2023/01/05 KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA MKUTANO WA TAREHE 30/08/2023, 31/08/2023 na 05/09/2023.**

5.1 Mihtasari hiyo iliwasilishwa kwenye mkutano.

5.2 Wajumbe waliipokea mihtasari hiyo na kuiridhia.

5.3 Mwenyekiti na Katibu waliweka saini na kuwa Kumbukumbu sahihi za mkutano baada ya kufanya masahihisho yafuatayo: -

5.4 Uk. Na. 6 Dondoo Na. 38.1 - 38.1.2 ya Muhtasari wa mkutano wa tarehe 30/08/2023.

Maelezo yaliyotolewa na Mhe. Mtamwega T. Mgaywa – Diwani wa Kata ya Kibara hayakuandikwa kwa usahihi hivyo mkutano uliagiza mhusika



CamScanner

ayawasilishe maelezo yake kwa maandishi ili yaandikwe kwa usahihi kwa ajili ya kumbukumbu za Halmashauri.

5.5 Uk. Na. 22 Muhtasari wa tarehe 05/09/2023.

- Chama cha ACT - isomeke Chama cha ACT Wazalendo.
- Kura 2 zilizoharibika isomeke kura 01 ya hapana na 01 iliharibika.

**MUHTASARI NA. HWB/2022 2023/01/06 KUPOKEA TAARIFA KUTOKA TARURA, MPANGO WA TANESCO NA RUWASA.**

6.1.1 **Taarifa ya utekelezaji wa shughuli za TARURA kwa kipindi cha robo ya I ya mwaka wa fedha 2023/2024**

6.1.2 Taarifa hiyo iliwasilishwa kwenye mkutano na Meneja TARURA (W) Eng. Baraka H. Mkuya kuwa, katika mwaka wa fedha 2023/2024, ofisi ya Meneja wa TARURA katika Halmashauri ya Wilaya ya Bunda iliidhinishiwa Bajeti ya matengenezo ya barabara yenye jumla ya thamani ya shilingi 3,856,246,800.28 kwa mchanganuo ufuatao: -

| | |
|---|---|
| - Matengenezo ya kawaida ya barabara | 781,594,500.29 |
| - Miradi ya Maendeleo (Tozo ya Mafuta) | 2,000,000,000.00 |
| - Miradi ya Maendeleo (Jimbo) | 1,000,000,000.00 |
| - Vyanzo vya Ndani vya Halmashauri | 00.00 |
| - Usimamizi na Utawala | 69,652,300.00 |
| - Kufanya tathmini ya hali ya barabara | 5,000,000.00 |
| **Jumla** | **3,856,246,800.28** |

6.1.3 **Mapokezi ya fedha.**

Kiasi cha shilingi 198,930,885.10 kati ya shilingi 3,856,246,800.28 sawa na asilimia 5.16 kilipokelewa hadi mwezi Novemba, 2023 kwa ajili ya kazi za matengenezo ya barabara. Kati ya fedha hizo shilingi 173,930,885.17 ni fedha za matengenezo ya kawaida ya barabara pamoja na utawala na usimamizi, shilingi 25,000,000.00 ni za ujenzi wa barabara kupitia fedha za tozo ya mafuta na shilingi 0.00 ni fedha za mfuko mkuu wa Serikali (Jimbo).

6.1.4 Wajumbe waliipokea taarifa hiyo, walijadili na kuipitisha baada ya kutoa ushauri: -

6.1.5 **USHAURI.** Kipaumbele cha matengenezo ya barabara katika mwaka wa fedha 2023/2024 kiwe katika barabara ambazo zilikuwa kwenye mpango wa mwaka 2022/2023 ambazo hazikufanyiwa matengenezo.

6.1.6 **USHAURI.** Matengenezo ya barabara yafanyike kufuatia mvua zinazoendelea kunyesha.

6.1.7 Aidha Meneja wa TARURA (W) Eng. Baraka H. Mkuya alitunukiwa zawadi ya cheti cha pongezi pamoja na shilingi 500,000.00 ambayo alikabidhiwa na Mkuu wa Wilaya Mhe. Vicent Anney ikiwa ni agizo la Baraza la Madiwani kwa kutambua utendaji kazi bora.



CamScanner

6.2 **Taarifa ya utekelezaji wa shughuli za TANESCO kwa kipindi cha robo ya I ya mwaka wa fedha 2023/2024.**

6.2.1 Taarifa hiyo iliwasilishwa kwenye mkutano na Ndg. Peter Selestine Meneja wa TANESCO (W) kuwa, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024 TANESCO Wilaya ya Bunda ilipata Bajeti ya kiasi cha shilingi 1,529,231,359 kwa ajili ya kutekeleza miradi pamoja na matengenezo ya miundombinu ya umeme. Bajeti ya shilingi 541,261,449 sawa na asilimia 35.39 kwa ajili ya kutekeleza miradi na shilingi 987,969,910 sawa na asilimia 64.61 ya matengenezo ya miundombinu ya umeme.

6.2.2 Aliendelea kueleza kuwa, TANESCO kupitia Mkandarasi M/s CHINA ELECTRIC SUPPLY COMPANY LIMITED inatekeleza mradi wa ujenzi wa njia kubwa ya umeme msongo wa Kilovolti 132 Bunda – Ukerewe pamoja na ujenzi wa kituo cha kupooza umeme cha Wilaya ya Ukerewe. Mradi huo unathamani ya shilingi Bilioni 131. Tayari hatua ya upimaji imekamilika na zoezi linaloendelea kwa sasa ni uthamini wa mali kwenye maeneo yatakayoathirika na ujenzi wa miradi.

6.2.3 Kuhusu mradi wa REA, jumla ya Vitongoji 33 viko katika hatua ya utekelezaji na tayari Mkandarasi Gizza Co. Ltd amekamilisha zoezi la upimaji. Vilevile Vitongoji 58 vitapata umeme kupitia mradi wa REA ujazilizi (DESIFICATION 2C) ambapo uhakiki wa eneo la mradi umefanyika na ujenzi unatarajiwa kuanza hivi karibuni. Pia REA ipo kwenye maandalizi ya kusambaza umeme kwenye Vitongoji vipatavyo 15 ambavyo ni mapendekezo ya Wabunge wote kutoka kila Jimbo. Mchakato mzima wa taratibu za kupata wazabuni ili kukamilisha kazi hiyo utafanyika kwa kipindi hiki mpaka Desemba, 2023 na mwezi Januari, 2024 Wakandarasi kwa ajili ya kutekeleza mradi huo watakuwa wanaanza kazi. Aidha kwa upande wa wateja tunaendelea kuwawashia kadri wanavyofanya malipo kwani kwa sasa vifaa vyote vinavyohusika na ujenzi wa umeme kwa wateja wapya vipo.

6.2.4 Alimaliza kwa kusema kuwa, TANESCO Wilaya ya Bunda inaendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali kupitia bajeti ya ndani ya Shirika ikiwa ni pamoja na kupeleka umeme Bunda DC, Mwibara area, Nampindi sekondari, Bulamba (sekondari ya wasichana), VETA Mahyolo etc.

6.2.5 Wajumbe waliipokea taarifa hiyo, waliijadili na kuipitisha.

6.3 **Taarifa ya utekelezaji wa shughuli za RUWASA kwa kipindi cha robo ya I ya mwaka wa fedha 2023/2024.**

6.3.1 Taarifa hiyo iliwasilishwa kwenye mkutano na Eng. William Boniphace Meneja wa RUWASA (W) kuwa, Halmashauri ya Wilaya ya Bunda inaendelea na utekelezaji wa miradi ya maji katika maeneo ya Wilaya ya Bunda kupitia program mbalimbali lengo ikiwa ni kuhakikisha wananchi wa Wilaya ya Bunda wanapata huduma ya maji safi, salama na yenye kutosheleza. Miradi iliyokamilika na inayoendelea kutekelezwa ni kupitia vyanzo vya maji vilivyopo Bunda kama Ziwa Victoria, Visima vifupi na virefu, Mabwawa na Chemichemi.



CamScanner

6.3.2 Alisema kuwa, kwa sasa hali ya upatikanaji wa maji kwa maeneo yanayohudumiwa na RUWASA imefikia 70.1% kati ya wakazi 389,450 waishio vjijini. Jumla ya wakazi 273,004 wanapata huduma ya maji. Miradi mbalimbali inatekelezwa ambapo ikikamilika itaongeza upatikanaji wa maji hadi kufikia 74 asilimia. Malengo ya RUWASA ni kuhakikisha ifikapo 2025 hali ya upatikanaji wa maji iweze kufikia 85 asilimia kama ilivyoainishwa kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi 2020 - 2025.

6.3.3 **Mikakati iliyopo katika kuhakikisha wananchi wa Wilaya ya Bunda wanapata maji safi na salama 2023/2024.**

(i) Ujenzi wa miradi ya maji katika Vijiji 47 (Jimbo la Bunda/Tarafa ya Chamriho 30 na Jimbo la Mwibara 17) ambapo chanzo kitakuwa Ziwa Victoria.
(ii) Ujenzi wa mradi wa maji wa Kijiji cha Ragata
(iii) Ukamilishaji wa mradi wa maji wa Hunyari
(iv) Ukamilishaji wa mradi wa maji wa Kabainja
(v) Kufanya utafiti na kuchimba visima katika maeneo ya Vijiji vya Mugeta, Kigaga, Namalebe na Kihumbu
(vi) Ujenzi wa mradi wa maji Mihingo kupitia Bwawa la Mihingo.
(vii) Kuendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa kulinda na kutunza miundombinu ya maji.
(viii) Kuendelea kuwahamasisha wananchi juu ya uchangiaji wa huduma ya maji ili miradi iweze kutoa huduma endelevu.

**Mpango wa maandalizi ya miradi ya mwaka 2023/2024 ikihusisha hali ya usanifu na maandalizi**

| JINA LA MRADI | CHANZO CHA FEDHA | GHARAMA | USANIFU |
|---|---|---|---|
| Kujenga miradi ya maji katika Vijiji 30 katika Jimbo la Bunda | NWF | 816,800,245.50 | 15% |
| Kujenga miradi ya maji katika Vijiji 24 katika Jimbo la Mwibara | PforR | 816,800,245.50 | 20% |
| Upanuzi wa mradi wa maji wa Nyamatoke hadi Kijiji cha Mihale | NWF | 390,666,785.00 | 100% |
| Ujenzi wa mradi wa maji wa Kijiji cha Ragata | PforR | 318,908,160.00 | 100% |

6.3.4 **Mipango kufikia 2025**

Aliendelea kutoa ufafanuzi kuwa, Wilaya imeweza kutekeleza miradi mbalimbali ya maji ikiwa na lengo la kuhakikisha kuwa wananchi wanapata



CamScanner

huduma ya maji safi na salama. Hadi kufikia Juni, 2025, jumla ya watu 284,802 sawa na asilimia 85 ya Wakazi wote waishio Vijijini katika Wilaya ya Bunda watakuwa wanapata huduma ya maji safi na salama na yenye kutosheleza.

6.3.5 Wajumbe waliipokea taarifa hiyo, waliijadili na kuipitisha.

6.3.6 Aidha kuhusu uendeshaji wa mradi wa maji Kibara, Meneja RUWASA (W) alisema kuwa kutokana na changamoto ya uendeshaji wa mradi wa maji Kibara ni vizuri Katibu wa mradi akawa ni mtaalam mwenye taaluma ya uhandisi wa maji kwa mujibu wa Taratibu kwa kuwa Kibara ni Mji unaokuwa.

6.3.7 Wajumbe waliujadili ushauri uliotolewa na Meneja RUWASA na mwisho kwa pamoja walikubaliana mradi wa maji Kibara uendeshwe chini ya Mamlaka ya Maji sambamba na mradi wa maji Nyamuswa kwa ustawi wa miradi hiyo.

**MUHTASARI NA. HWB/2022 2023/01/07 KUPOKEA TAARIFA YOYOTE AMBAYO MWENYEKITI ANAPENDA ITOLEWE KWA HALMASHAURI.**

7.1 Hapakuwepo na taarifa kutoka kwa Mwenyekiti wa Halmashauri.

**MUHTASARI NA. HWB/2022 2023/01/08 KUPOKEA TAARIFA ZA KAMATI ZA KUDUMU ZA HALMASHAURI KUTOKA KWA WENYEVITI WA KAMATI AMBAO WATAHUSIKA KUJIBU MASWALI YA WAJUMBE KUHUSIANA NA KAZI ZA KAMATI HUSIKA.**

8.1 **Taarifa ya Kamati ya Kudhibiti UKIMWI (W).**

8.1.1 Taarifa hiyo iliwasilishwa kwenye mkutano na Mwenyekiti wa Kamati.

8.1.2 Wajumbe waliipokea taarifa hiyo, waliijadili na kuipitisha.

8.2 **Taarifa ya Kamati ya Maadili ya Madiwani**.

8.2.1 Taarifa hiyo iliwasilishwa kwenye mkutano na Mwenyekiti wa Kamati.

8.2.2 Wajumbe waliipokea taarifa hiyo, waliijadili na kuipitisha

8.3 **Taarifa ya Kamati ya Huduma za Uchumi.**

8.3.1 Taarifa hiyo iliwasilishwa kwenye mkutano na Mwenyekiti.

8.3.2 Wajumbe waliipokea taarifa hiyo, waliijadili na kuipitisha.

8.4 **Taarifa ya Kamati ya Huduma za Jamii.**

8.4.1 Taarifa hiyo iliwasilishwa kwenye mkutano na Mwenyekiti.

8.4.2 Wajumbe waliipokea taarifa hiyo, waliijadili na kuipitisha.

8.5 **Taarifa ya Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango.**

8.5.1 Taarifa hiyo iliwasilishwa kwenye mkutano na Mhe. Brown Mborwe kwa niaba ya Mwenyekiti.

8.5.2 Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na waliijadili kwa kutoa hoja mbalimbali ambazo zilitolewa ufafanuzi na Mkurugenzi Mtendaji (W). Aidha baadhi ya hoja hizo ni pamoja na:-



CamScanner

### 8.5.3 Utekelezaji na usimamizi wa miradi ya maendeleo.

Mkurugenzi Mtendaji (W) alisema kuwa yapo mabadiliko makubwa katika utekelezaji wa miradi ukilinganisha na awali japokuwa ipo baadhi ya miradi isiyokamilika. Alirejea wakati anafika katika Halmashauri hii alikuta ujenzi wa jengo la Utawala upo hatua ya msingi na kuwa vifaa vingi vilikuwa vimelipiwa lakini havipo katika eneo la mradi. Alilazimika kusitisha ujenzi kwa miezi 03 ili Halmashauri ijipange kujua vifaa vitapatikanaje pamoja na changomoto pia ya mvua iliyosababisha kufukia msingi na kulazimika kuondoa udongo ili mradi uendelee. Alishiriki kumtafuta Mtaalamu Mshauri ambaye anatekeleza kwa shilingi Milioni 91,229,800 anayetambulika kwa jina la BICO ambaye ana uwezo pia wa kulipa fidia endapo itajitokeza changamoto katika mradi lakini alikuta kuna mtaalam wa TARURA (W) Eng. Kassimu aliyeomba kutenda kwa shilingi Milioni 120 licha ya kuwa yeye ni mtumishi wa Serikali. Pamoja na juhudi zote hizo mpaka kuhakikisha wazabuni wanarejesha fedha na kuleta vifaa licha ya mzabuni moja kuendelea kudaiwa lakini alionesha masikitiko yake kwa kauli za wajumbe kuhusu kushindwa kusimamia miradi.

### 8.5.4 Changamoto za Mradi wa Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi

Alizungumzia changamoto za Mradi wa Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi ambapo alisema kuwa anawajibika kwa makosa yanayofanywa na watumishi lakini siyo yote. Alisema kuwa baada ya kuona mradi huo hauendi sawa aliishauri Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango kumuondoa Mratibu huyo lakini wajumbe wake walimpinga na kumdhalilisha mbele ya aliyekuwa Mratibu wa Mradi huo kwa maelezo kuwa ana maslahi binafsi. Alipokea pia barua kutoka katika ofisi ya Mkuu wa Wilaya kuhusu kutomuondoa Mratibu huyo kuwa Mratibu wa mradi. Alisema kuwa aliandika barua kupeleka mkoani kuhusu changamoto za Mratibu lakini aliambiwa arudi nayo na wao hawawezi kufanya chochote zaidi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) kumchukulia hatua, aliomba hata ahamishwe lakini Mkoa haukukubali. Alisema kuwa anastaajabu kuona wajumbe hawaoni kama Mratibu anahusika katika chagamoto za mradi wakati hivi karibuni walimuagiza Mkurugenzi Mtendaji (W) amuondoe kuwa Mratibu na katika mkutano huo hawakuona kama ana makosa ili Mratibu aliyepo awajibike kwa changamoto ikiwa ahusiki.

### 8.5.5 Changamoto za Watendaji wa Kata na Vijiji

Alikiri uzembe unaofanywa na Watendaji licha ya kushirikishwa mara wa mara katika masuala ya mapato na usimamizi wa miradi. Alisema kuwa, endapo wajumbe watahitaji kila Mtendaji mwenye changamoto jina lake liwasilishwe kwenye mkutano wa Baraza kwa ajili ya kufukuzwa/kuchukuliwa hatua atafanya hivyo.

### 8.5.6 Kizuizi cha Mugeta kutokusanya mapato.

Alisema kuwa changamoto hiyo ingekuwa imefanyiwa kazi mapema kama ingekuwa imewasilishwa kwa wakati kwani mkusanyaji kwenye kizuizi hicho anajulikana. Aliwaomba wajumbe wasaidie kubaini sababu za geti hilo kutokusanya.

.5.7 **Mifuko ya saruji iliyoazimwa na shule ya sekondari Sunsi.**

Alisema kutokana na hoja hiyo kujirudia mara kwa mara amejipanga na wataalamu wake kuanza kulipa mifuko hiyo ya saruji. Hata hivyo mifuko hiyo wanayokwenda kuilipa ilipasuka kufuatia ajali ya gari iliyokuwa imebeba mifuko 400 na mifuko karibu 100 ilipasuka na watu 02 walifariki katika ajali hiyo wakati inapelekwa katika shule ya sekondari Sunsi.

3.5.8 Alihitimisha kwa kusema kuwa, kukaa kwake katika Halmashauri ya Wilaya ya Bunda kuna mengi mazuri na makubwa aliyofanya na yupo tayari kupokea maamuzi yoyote ya Baraza la Madiwani yatakayoamuliwa dhidi yake.

8.6 **Nasaha za viongozi.**

8.6.1 **Nasaha kutoka kwa Mkuu wa Wilaya - Mhe. Vicent Anney.**

8.6.2 **Taarifa ya ukaguzi wa mradi wa ujenzi wa shule ya sekondari ya wasichana.**

Alimpongeza Mkurugenzi Mtendaji (W) kwa kuwasilisha taarifa ya ukaguzi wa mradi wa ujenzi wa shule ya sekondari ya wasichana kwa wakati kwani mara nyingi Halmashauri hazipendi kuwasilisha taarifa za ukaguzi wa ndani katika ofisi ya Mkuu wa Wilaya pia alimpongeza Mkaguzi wa Ndani kwa taarifa iliyowasilishwa.

8.6.3 **Uboreshaji wa Sheria ndogo za Vijiji.**

Alisisitiza kuboreshwa kwa Sheria ndogo za Vijiji ili kuongeza vipengele vifuatavyo: -

- Wananchi kuhudhuria vikao vya kisheria pamoja na vikao vya viongozi vinapoitishwa.
- Chakula shuleni.
- Kila mwananchi anawajibika kulinda wanyama wake hivyo Mkurugenzi Mtendaji (W) apitishe "operation" ya mbwa pamoja na nguruwe wote wanaozurura ovyo mtaani.

8.6.4 **Usimamizi wa elimu shuleni.**

Alihitaji kuwepo na kikao kazi na walimu kabla shule hazijafunguliwa. Alisema kuwa kufikia shule kufunguliwa asiwepo mtoto anayekaa chini hivyo walimu washirikiane na wazazi kutekeleza hilo. Alizungumzia pia changamoto ya Wanafunzi kutokujua Kusoma, Kuandika na Kuhesabu inavyoathiri ufaulu wa wanafunzi sambamba na kukosekana kwa mpango kazi kwa walimu.

8.6.5 **Utendaji kazi wa Kamati ya Fedha, Uongozi Mipango.**

Alisema kuwa Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango hukutana kila mwezi ikihusisha Wenyeviti wa Kamati zote za Kudumu, Wabunge wote, pamoja na Katibu Tawala (W) ambaye pia ni mjumbe wa vikao vya CMT. Alisema kuwa Kamati hiyo ikifanya vizuri kwa maana ya kusimamia mapato, makusanyo yataongezeka pia hakuna mradi utakoharibika. Aliwapitisha pia wajumbe katika majukumu mbalimbali ya Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango.

Aidha alisema kuwa madaraka ya Kamati hii ni kama ya Kamati zingine za Kudumu na hivyo hairuhusiwi kisheria kufanya kazi/majukumu ya Kamati zingine za Kudumu. Kwa ujumla, majukumu yake ni pamoja na kusimamia na



CamScanner

kudhibiti ukusanyaji wa mapato na matumizi ya mali ya Halmashauri kwa kupitia vikao vyake.

**8.6.6 Usimamizi wa miradi.**

Alisema kuwa Halmashauri hii imekuwa na historia mbovu ya usimamizi wa miradi hasa yenye gharama kubwa kuanzia shilingi Milioni 400 kwa watu kutaka kujinufaisha. Taratibu hazifuatwi makusudi ili kurahisisha wizi kwenye miradi. Aliwaahidi wajumbe kwenye uongozi wake hakuna mradi utakaoharibika hivyo wataalam wajipange kwa hilo. Alikemea suala la ununuzi wa vifaa vingi kupita kiasi akitolea mfano katika ujenzi wa mradi wa jengo la utawala, mpaka tarehe ya mkutano bado kuna shilingi Milioni 117 zipo nje kwa makosa hayo ya kutofuata taratibu. Alisema kuwa Mkurugenzi Mtendaji (W) hahusiki kwa changamoto yoyote inayojitokeza katika utekelezaji wa miradi kwani vifaa vikishanunuliwa mwenye jukumu la kusimamia ni wataalam waliosomea.

**8.6.7 Uchukuaji wa hatua kwa watumishi wasiotekeleza majukumu yao.**

Alimuomba Mkurugenzi Mtendaji (W) apunguze kuwalea watumishi wote wasiotekeleza majukumu yao. Alisisitiza kila mtumishi awe na mpango kazi hasa kwa wale wanaosimamia miradi ya maendeleo.

**8.6.8 Suala la Diwani wa Kata ya Hunyari kupigwa na aliyekuwa Mratibu Elimu Kata.**

Alisema kuwa suala hilo ni la kijinai hivyo liripotiwe kwenye vyombo vya Dola.

**8.6.9 Changamoto za Mradi wa kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi.**

Alisema kuwa wakati anakuja Wilaya ya Bunda alikuta mradi wa mazingira una changamoto. Barua yake aliyomwandikia Mkurugenzi Mtendaji (W) ya kumuondoa Mratibu huyo ni baada ya kutembelea mradi huo na kubaini mapungufu kadhaa. Alisema kuwa Mkuu wa Wilaya aliyepita ndiye aliyeagiza aliyekuwa Mratibu wa Mradi asiondolewe.

**8.6.10 Upotevu wa mifuko 640 ya saruji.**

Alisema kuwa mifuko ya saruji 640 iliyokamatwa ni mali ya Halmashauri ya Wilaya ya Bunda. Saruji hiyo iliagizwa ishushwe Guta na mpokeaji aliipokelea Guta. Mifuko hiyo atakabidhiwa Mkuu wa Wilaya na ataona aigawe katika Taasisi gani. Aidha alisema kuwa wanaendelea pia kufuatilia mifuko mingine 1280 ambayo inaonekana iliingia Wilaya ya Bunda lakini haijulikani ilishushwa wapi.

**8.7 Nasaha kutoka kwa Katibu Tawala (M).**

Bw. Songoma S. Pius Mwakilishi wa Katibu Tawala Mkoa, alimshukuru Mwenyekiti kwa jinsi alivyoendesha mkutano huo. Aliwaomba Wahe. Madiwani kuyaishi yale yote yaliyozungumzwa na viongozi mbalimbali. Alisisitiza ushirikiano baina ya Mkurugenzi Mtendaji (W), Mwenyekiti wa Halmashauri, Wahe. Madiwani na watumishi wote kwa maslahi mapana ya Halmashauri. Alihitimisha kwa kusema kuwa "timu inayocheza pamoja hushinda pamoja".



CamScanner

**MUHTASARI NA. HWB/2022 2023/01/09 KUPOKEA TAARIFA KUTOKA KWA MKURUGENZI MTENDAJI (W)**

9.1 Taarifa hizo zilijadiliwa faragha baada ya wajumbe kujigeuza Kamati.

9.2 Hata hivyo baada ya majadiliano yaliyofanyika faragha kwa mujibu wa Kanuni 36 na 37 ya kanuni za Kudumu za Halmashauri 2020, Mwenyekiti alisoma maamuzi ya Kamati nzima ya Halmashauri kama ifuatavyo: -

| NA. | JINA LA MTUHUMIWA | HATUA ZILIZOCHUKULIWA | SABABU ZA KUCHUKULIWA HATUA |
|---|---|---|---|
| 1.<br>2.<br>3. | Mwl. Joseph Washington - Mwl. Shule ya sekondari Bulamba<br>Bw. Ibrahim Makuli - Mtendaji wa Kata ya Butimba<br>Mwl. Abinel Wegero - Afisa Elimu Kata Butimba | Afunguliwe mashauri ya nidhamu na asimamishwe kazi kupisha uchunguzi. | Upotevu wa mifuko 3498 ya saruji katika mradi wa shule ya wasichana Mara ambapo: -<br><br>Mifuko 2220 ya saruji haikuingizwa kwenye leja pamoja na kuwa ililipiwa na kupokelewa<br><br>Mifuko 1278 ya saruji ambayo ilitolewa kwenye leja ikionesha wamepewa mafundi ujenzi na wafyatuaji wa tofali lakini hawakusaini katika daftari kuthibitisha kupokea. |
| 4. | Bw. Peter Pugiri - Afisa Manunuzi | Afunguliwe mashauri ya nidhamu na achunguzwe akiwa kazini | Upotevu wa mifuko 3498 ya saruji katika mradi wa shule ya wasichana Mara ambapo; -<br><br>Mifuko 2220 ya saruji haikuingizwa kwenye leja pamoja na kuwa ililipiwa na kupokelewa<br><br>Mifuko 1278 ya saruji ambayo ilitolewa kwenye leja ikionesha wamepewa mafundi ujenzi na wafyatuaji wa tofali lakini hawakusaini katika daftari kuthibitisha kupokea. |
| 5. | Ndg. Dickson Balige - Aliyekuwa Mratibu wa mradi wa Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabia Nchi (BCRAP) | Afunguliwe mashauri ya nidhamu na asimamishwe kazi kupisha uchunguzi | Kushindwa kusimamia kikamilifu mradi wa Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabia Nchi (BCRAP) ikiwa ni pamoja na kutozingatia ushauri wa kitaalam wakati wa uchimbaji wa mabwawa 10 ya ufugaji wa samaki katika kijiji cha Mchigondo na Isanju |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 6. | Ndg. Emmanuel Sulo -Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi na Ugavi (W) | Afunguliwe mashauri ya nidhamu na asimamishwe kazi kupisha uchunguzi | Kushindwa kusimamia taratibu za manunuzi katika mradi Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabia Nchi (BCRAP) zikiwemo za ununuzi wa samaki, uchimbaji wa mabwawa ya ufugaji wa samaki katika Kijiji cha Mchigondo na Isanju ambapo uchimbaji ulifanyika pasipo kuwepo nukuu za bei. |
| 7. | Timu nzima ya awali ya usimaizi wa mradi wa Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabia Nchi (BCRAP) | Wapewe barua za onyo | Kushindwa kushiriki kikamilifu katika usimamizi wa mradi wa Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabia Nchi (BCRAP) |
| 8. | Ndg. Stephen Ochieng - Afisa Uvuvi | Taratibu za kiutumishi ziendelee | |
| 9. | Ndg. Hussein Kichwabuta - Mtendaji wa Kata | | |
| 10. | Watumishi 20 walioanzishiwa Kamati za Uchunguzi | Taratibu za kiutumishi ziendelee | |
| 11. | Ndg. Mfaume Majuto – Afisa Uvuvi | Apewe barua ya onyo | Kuidanganya Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango kuwa alihesabu vifaranga vya samaki wazazi vilivyoletwa na Ruvu 832 KJ na kukuta idadi ya samaki 1000 na kusaini hati ya mapokezi na baada ya mahojiano zaidi alikiri kutohesabu. |

**MUHTASARI NA. HWB/2022 2023/01/10 KUFUNGA MKUTANO.**

10.1 Katibu alimkaribisha Mwenyekiti afunge mkutano

10.2 Mwenyekiti wakati akifunga mkutano alisisitiza kuwa maamuzi ya Baraza la Madiwani yazingatiwe.

10.3 Alifunga mkutano saa 12:58 jioni.

**UMETHIBITISHWA**

SAINI YA KATIBU........................SAINI YA MWENYEKITI..........................................

JINA LA KATIBU CHAUSSA M. MKWAWA ........JINA LA MWENYEKITI CHARLES M. MANUMBEI ..........................

TAREHE 16.02.2024 ..............